HAKIARDHI

# ARDHI NI UHAI

ISSN NO. 0856-9495 TOLEO LA 2 SEPT - DES 2004

YALIYOMO

Marekebisho ya mfumo wa umiliki ardhi 1
Tahariri 2
Buyuni wakataa kuburuzwa 4
Wananchi Hanag wapinga kubinafsishwa kwa ardhi yao 5
Marekebisho ya 14 ya Katiba na haki ya kumiliki mali 8
Machapisho 11

## NUKUU YA LEO

*"Kwa watu ambao walikuwa watumwa, au ambao walikuwa wakionewa, na kunyanyaswa kwa sababu ya Ukoloni, Ukabaila, au Ubepari, "maendeleo" maana yake ni "ukombozi". Kitendo chochote kinachowapa uwezo zaidi wa kuamua mambo yao wenyewe, na kutawala maisha yao wenyewe, ni kitendo cha maendeleo, japo kama hakiwaongezei afya wala shibe."*

**Mwangozo wa TANU 1971**

# MAREKEBISHO YA MFUMO WA UMILIKI ARDHI TANZANIA:

## *Yanalinda Maslahi ya Nani?*

*Na*
*Salma Maulidi*

Mwaka 1999 kulitokea mabadiliko makubwa katika mfumo wa umilikaji ardhi nchini. Sheria mpya ya ardhi ilipitishwa kufuatia sera mpya ya ardhi ya mwaka 1995. Mabadiliko haya yalianzisha itikadi mpya si tu katika mfumo wa umilikaji ardhi bali pia katika mtizamo mzima wa jinsi ya kuleta maendeleo nchini. Mapema mwaka huu sheria hiyo ya ardhi imerekebishwa tena.

### Usuli wa Marekebisho ya 2004.

Marekebisho ya Sheria ya Ardhi yaliyofanywa mapema mwaka 2004 yalikuwa kwenye masuala makuu mawili. Awali ya yote marekebisho haya yanaingiza dhana ya *kuuza ardhi tupu*, kinyume na ilivyokuwa huko nyuma. Na pili sheria inafanyiwa marekebisho kwenye sehemu iliyohusiana na kuweka ardhi rehani. Kwa sababu uwekaji ardhi rehani utawalimbikizia wengi madeni hasa ukizingatia vipato vya chini vya wananchi walio wengi, viwango hafifu vya



*Mshiriki katika Warsha ya Haki za Ardhi Wilayani Hanang akisisitiza haja ya kulinda maslahi ya ardhi ya wanyonge.*

Inaendelea Uk.3

**Ardhi ni Uhai** ni jarida la HAKIARDHI ambalo hutolewa mara tatu kwa mwaka. Kusudi kubwa ni kuwapa wadau wa Taasisi hii taarifa mbalimbali zinazohusiana na mambo ya ardhi.

**Mchapishaji**
HAKIARDHI

**Mhariri**
Yefred Myenzi

**Bodi ya Wahariri**
Ng'wanza Kamata - M/Kiti
Yefred Myenzi - Mhariri
Abdallah Matata - Mjumbe
Rehema Mfaume - Mjumbe

**Mchapaji**
Ecoprint Ltd.

## UJUMBE WA BODI KWA WASOMAJI

Wasomaji wa jarida hili wanakaribishwa kutoa michango yao kwa kuuliza maswali au kwa kuandika makala. Maswali, Maoni na Makala (zisizozidi kurasa tatu) zitumwe kwa Mhariri kupitia anuani ifuatayo:

Mhariri:
Ardhi ni Uhai
S.L.P. 75885
Dar es Salaam

Email:
editor@hakiardhi.org

# TAHARIRI

Kasi ya marekebisho ya mfumo wa uchumi wa Tanzania imeendelea bila kusita. Kasi hii inatarajiwa kuendelezwa na Serikali iliyopo na ile ijayo baada ya hii. Kilicho wazi ni kuwa katika kuendeleza mabadiliko haya hoja na kelele za 'walevi' wasioona na kusifia faida zitokanazo na zilizokwisha patikana kutokana na marekebisho haya ya uchumi zitaendelea kupuuzwa. Pamoja na hali hii si vibaya kuendelea kujiuliza swali je mabadiliko haya yanayotokea yanamfaidisha nani?

Mathalani hatua zote za ubinafsishaji wa mashirika mbalimbali ya umma sio tu zilipingwa vikali na wananchi wakiongozwa na wafanyakazi wa mashirika hayo. Pamoja na kupuuzwa kwa waliohoji kubinafsishwa kwa mashirika hayo na kuahidiwa kuona faida baada ya kuvuta subira swali linabaki je mashirika ya huduma za maji, simu, umeme n.k. yaliyobinafsishwa au kukodishwa yanatoa huduma bora zaidi leo kuliko kabla hayajabinafsishwa? Kama sivyo ni nani anafaidika na ubinafsishaji huo? Yawezekana wapo, lakini ni kina nani hao na ni wangapi?

Ni kutokana na hali hii na dhamira ya Serikali kuendeleza ubinafsishaji wa kila kinachowezekana tunapata wasiwasi juu ya hatua mbalimbali za kisera na kisheria ambazo zinachukuliwa na Serikali. Kwa mfano, kwa hoja ya kupunguza umasikini, Serikali imelegeza masharti ya umilikaji na uhamishaji ardhi (Kwa mujibu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Ardhi 2004). Na hivi sasa Serikali inaendesha zoezi la usajili na urasmishaji wa mali 'mfu', kwa ushauri wa Mtaalamu wa Kiperu, kama mkakati wa kupunguza umasikini. Katika hatua zote hoja inayojengwa ni kuwa kama masikini wakiwezeshwa kupata mitaji toka katika mabenki basi watakuwa wamepatiwa fursa ya kujiondolea umasikini. Pengine ni kweli masikini, hasa wakulima wanahitaji mikopo. Lakini swali la kujiuliza ni mikopo ya aina gani, kwa ajili ya nini na kwa masharti gani? Ikiwa mabenki ya biashara yaliyopo hapa nchini yataanza kuwakopesha wakulima na kwa masharti na riba zilizopo, na wakulima wadogo wakashawishika kuchukua mikopo kwa masharti yaliyopo ni wazi watakuwa wameamua kujitia kitanzi wao wenyewe.

Hili likitokea halitakuwa linasigana na mfumo kwa vile kimantiki mfumo wa uchumi ambao Serikali ya sasa inautetea na kuujenga umejisimika kwenye misingi ya kujenga na kuimarisha matabaka. Kwa asili, mfumo huu hufaidisha na kutajirisha wateule wachache na kufukarisha walio wengi. Hata hivyo mfumo huu umejaa hila na ulaghai mwingi na una uwezo mkubwa wa kutoa matumaini hewa kwa masikini. Lakini ukweli unabakia kuwa mfumo na hatua zinazochukuliwa zinafungua milango zaidi ambayo matokeo yake ni ufukara zaidi hasa kwa wanavijiji wanaomiliki ardhi na kuitumia kama rasilimali muhimu kwa ajili ya kuzalisha chakula na ziada kidogo kwa ajili ya kujikimu na ustawi wao. Kwa kutambua hasara na hatari zilizofichika ndani ya mfumo huu wananchi fukara, wa mijini na vijijini, hawana budi kuchukua hadhari kubwa, aidha ni muhimu kwao wakishirikiana na wananchi wengine kuendelea kujielimisha, kujadili na 'kuumbua' mfumo huu na hatua zinazoendana nao ili waweze kulinda uhuru na utu wao.

Inatoka Uk.1

marudisho na nguvu ya ununuzi. Hakika kuna uwezekano mkubwa kwa mwananchi kupoteza si tu ardhi yao bali pia akiba yoyote waliyojiwekea. Pia kuna uwezekano wa kutawala kwa rushwa ambapo wakubwa watajitahidi kujizatiti kiuchumi na ikiwezekana hawatasita kutumia madalali kujinufaisha kutokana na shida za wengine.

Ni jambo dhahiri pia kwamba wanachi wengi wanamiliki maeneo madogo sana, na taasisi za fedha hazipendelei kutoa mikopo kwa maeneo kama haya kwani huwa hayaambatani na upatikanaji wa faida. Ni jambo la kawaida na linalofahamika sana kuwa wakulima hukopeshwa na Vyama vya Wakulima au vya Ushirika. Kwa bahati mbaya hapa nchini taasisi hizi zimedhoofishwa na mfumo mpya wa kiuchumi. Bila ya shaka mabadiliko haya hayawezi kuwa na manufaa kwa wakulima. Na baadhi ya wasomi wanafananisha hoja zinazotetea mabadiliko haya na hali iliyotokea ilipopitishwa Sheria ya Udhibiti wa Kodi ya mwaka 1984 kwa kigezo cha kuwatetea wanyonge dhidi ya mabwana lakini ikaja kubainika kwamba kiutendaji inawalinda zaidi wenye nyumba na matajiri na wala si wapangaji ambao badala yake walijikuta wakitishiwa na uwezekano wa kutolewa nje.

Mageuzi yaliyofanyika katika mfumo wa umilikaji ardhi ni mlolongo wa mabadiliko katika sekta mabalimbali kwa nia ya kuuimarisha uchumi wa Tanzania. Katika juhudi za makusudi zenye lengo la kuweka mazingira mazuri kwa ajili ya wawekezaji wa kigeni serikali ya Tanzania imelazimika kuchukua hatua mbalimbali kuwavutia wawekezaji ikiwemo kurahisisha upatikanaji na uhamishaji ardhi.

Azma ya kuifanya ardhi kama bidhaa inayohamishika na kununulika inaelezwa bayana na Rais Benjamin Mkapa, kama alivyonukuliwa akisema kuhusu ardhi, "ardhi huleta fursa ya uwezekaji ...ni bidhaa inayoweza kuwekewa mkopo...ni rasilimali katika sekta ya ufugaji...inaweza kutumika katika ubia wa viwanda...kuanzishwa nchini Tanzania".

Kwa mujibu wa Dr. Kapinga mfumo wa ardhi unailenga sekta yenye uwezo wa kifedha na uwezo wa kuwekeza katika viwanda. Hata hivyo, sehemu kubwa ya mali ya asili nchini iko katika ardhi ya vijiji. Matarajio ni kwambamatumizi ya rasilimali hizi yana uhusiano wa moja kwa moja na jinsi ardhi ya vijiji inavyomilikiwa na kutumika hivyo kuweka umuhimu wa kipekee katika suala la ardhi na demokrasia.

> ***"Ardhi huleta fursa ya uwekezaji... ni bidhaa inayoweza kuwekewa mkopo ... ni rasilimali katika sekta ya ufugaji... inaweza kutumika katika ubia wa viwanda...***

Aliyekuwa mwenyekiti wa Tume ya Rais ya Ardhi, Prof. Issa Shivji analielezea lengo la mfumo mpya wa ardhi kuwa ni kubinafsisha mfumo wa umiliki ardhi kwa nia ya kurahisisha uuzaji na uhamishaji wa mali isiyohamishika. Hivyo, kumekuwa na haja ya kubadilisha taratibu za kisheria na za kiutawala ikiwemo mfumo wa kusimamia, kugawa na kuandikisha ardhi ili ziendane na matakwa ya mfumo wa uchumi huria. Mkazo umewekwa katika kuihamisha ardhi na si kuwahakikishia wananchi milki yao ya ardhi.

### Itikadi mpya?

Baadhi ya mabadiliko katika mfumo yametokana na mabadiliko ya kiitikadi na kisiasa. Marekebisho ya sheria ya ardhi yaliyofanyika mwaka 2004 yanaingiza dhana mpya ya kuuza ardhi tupu. Kwa kufanya hivi dola inatimiza lengo la kukidhi matakwa ya kiuchumi kwa kuandaa sheria itakayo rahisisha mikopo, uwekaji rehani na uhamishaji wa hati miliki.

Mfumo mpya wa umiliki ardhi unaleta uhasama kati ya dola na wananchi kwa vile unawezesha kuporwa kwa kitega uchumi pekee walichonacho wananchi yaani ardhi. Wakati huo huo serikali imekuwa inashindwa kuwapatia wananchi ruzuku ili waweze kuendeleza shughuli zao za kilimo na biashara. Mtafiti jamii Bi. Marglin anaona kwamba msisitizo wa faida na ubinafsi katika mfumo mpya wa ardhi unadhoofisha ada zilizojengeka katika jamii kwa vile huonekana ni kikwazo kwa mafanikio ya kiuchumi. Pia, kushindwa kwa siasa za *Ujamaa* nchini kumeathiri kwa kiasi kikubwa mitizamo juu ya utawala shirikishi na rasilimali.

*Hapana shaka, sheria mpya inaukumbatia ubepari kinaganaga, na kwa kufanya hivi, inaleta*

Inaendelea Uk.10

## UTWAAJI WA ARDHI VIJIJINI:

# BUYUNI WAKATAA KUBURUZWA

Buyuni II kama vilivyo vijiji vingine nchini kiliandikishwa rasmi kama kijiji cha ujamaa tarehe 24/08/1980 na kupewa hati ya usajili Namba DSM/Kij/46. Kijiji hiki kipo katika eneo linalopakana na vijiji vifuatavyo; Chanika upande wa Kusini, Msongola upande wa Mashariki, Pugu Mwakanga upande wa Kaskazini, na upande wa Magharibi ipo Hifadhi ya Msitu wa Kazimzumbwi.

Wakazi wengi wa kijiji hiki ni wakulima wanaotumia zana duni za kilimo katika ardhi nzuri yenye rutuba iliyo kwenye umbo la nchi tambarare na miinuko kiasi.

Kwa rasilimali zilizomo kijijini hapa haiyumkiniki kijiji hiki kufananishwa na Buyu la Asali. Ukweli huu unatokana na kijiji hiki kuwa kivutio kikubwa kwa watu wenye maslahi mbalimbali, hasa, kwenye ardhi ya kijiji. Kwa hivyo wakazi wa kijiji hiki kwa zaidi ya muongo mmoja hivi sasa wamekuwa katika ukinzani mkubwa na watu na mamlaka mbalimbali ambazo zimekuwa zikikodolea macho ardhi ya kijiji hiki.

Kwa bahati mbaya zaidi viongozi waliopo hivi sasa kijijini hapa, pamoja na kuwa wamechaguliwa na wananchi, uongozi wao umewapa Kisogo wananchi. Hii ni kutokana na ukweli kwamba wao wamekumbatiwa na kushikamana na uongozi wa Wilaya na Manispaa kuhujumu maslahi na haki za wananchi na kunyakua na kupora ardhi ya wanakijiji wa Buyuni. Kwa muda sasa kumekuwa na matukio mbalimbali ya uvamizi na majaribio ya kupora ardhi ya wanakijiji wa Buyuni II hatua ambazo zimepingwa vikali na wananchi. Baadhi ya matukio hayo yanatajwa na kujadiliwa katika sehemu ifuatayo ya makala hii.

Mwaka 2000 ardhi ya kijiji cha Buyuni II ilivamiwa. Uvamizi huu uliendeshwa na kusimamiwa na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ilala. Uvamizi huu ulionekana kuwa ulikuwa umeandaliwa vyema kwa vile uliambatana na polisi waliokuwa wamejipanga na kujiandaa kukabiliana na lolote litakalojitokeza. Uvamizi huu ulidaiwa kufanywa kwa niaba ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Inavyoonekana, uvamizi huu haukuwa umezingatia wala kuheshimu misingi ya sheria, kanuni na taratibu.



*Mjadala juu ya ardhi umehusisha makundi na njia mbalimbali ikiwemo sanaa*



*Paul Jed*

'Wavamizi' walianza zoezi la kupima viwanja kwenye makazi ya wanakijiji bila ridhaa yao na bila makubaliano yoyote kati ya wanakijiji na Serikali au Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Wananchi ambao walihoji utaratibu huo walitishwa na mwanakijiji mmoja aliyeamua kuzuia zoezi hilo katika ardhi yake alileteva askari mwenye silaha na chini ya ulinzi wa askari huyu enao lake likapimwa viwanja.

Japokuwa upimaji wa viwanja ulifanyika kwa mabavu wananchi wa Buyuni II hawakuridhika na hivyo waliamua kujaribu kutumia njia zingine kulinda haki zao. Walijaribu kupata ushauri wa kisheria na kuchukua hatua za kisheria bila mafanikio; wakaviona vyombo vya habari ambavyo, kwa kiasi fulani vilisaidia kutangaza na kuonesha madhira waliyoyapata wanakijiji kutokana na zoezi hilo. Katika jitihada zote hizi Serikali ya kijiji ilijiweka pembeni utadhani vile yaliyokuwa yakitokea hayakuwahusu.

Upinzani wa wananchi dhidi ya uvamizi, na mchango wa vyombo vya habari uliifanya Serikali ya Wilaya, ikishirikiana na serikali za kijiji na Manispaa kutafuta njia za kupoza mambo. Njia moja waliyotumia ni kuitisha mkutano kijijini Buyuni II. Katika Mkutano huo, ambao ulihudhuriwa na Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Kamanda wa Polisi wa Wilaya (OCD) na viongozi wengine, pamoja na wanakijiji cha Buyuni ulihutubiwa na Mkuu wa Wilaya ambaye pamoja na kukiri kuwa makosa yalikuwa yamefanyika katika kuvamia kijiji cha Buyuni aliwaasa wananchi wakubaliane na zoezi zima la upimaji viwanja katika maeneo yao. Aidha Mkuu wa Wilaya aliomba radhi kwa makosa yaliyokuwa yametendeka.

*Inaendelea uk. 9*

# WANANCHI HANANG WAPINGA KUBINAFSISHWA KWA ARDHI YAO

Miongo zaidi ya miwili imepita toka Serikali itwae ardhi ya wawanavijiji wa kata za Basutu, Gehandu na Laghanga katika wilaya ya Hanang. Ardhi hiyo ilitwaliwa kwa ajili ya kuanzisha kilimo cha Mashamba makubwa ya ngano. Wakati ule wa utwaaaji wananchi walipinga vikali hatua ya kupokonywa ardhi yao. Upinzani wa wananchi dhidi ya maamuzi haya ya Serikali yaliyofanywa kwa hoja ya manufaa ya umma, ulichukua sura mbalimbali ikiwa ni pamoja na kugoma kuhama katika eneo lililotakiwa – jambo ambalo lilikabiliwa na matumizi makubwa ya nguvu za dola. Lakini pia kupinga huko kwa wananchi kulichukua sura ya kufungua kesi mahakamani pindi ilipodhihirika wazi kwao kuwa uwezo wao wa kushindana na nguvu za dola ulikuwa mdogo. Baadhi ya kesi zilishamalizika na nyingine zingali mahakamani zikidai haki ya umiliki wa ardhi iliyopokonywa toka kwao na kutwaliwa na Serikali kwa ajili ya shirika la NAFCO.

Mradi wa kilimo cha mashamba makubwa ya ngano chini ya NAFCO umeshindwa na kiasi kikubwa cha ardhi kimekuwa hakitumiki kwa miaka mingi sasa. Kwa kuona hali hiyo baadhi ya wananchi, kwa kusukumwa na shida na mahitaji ya ardhi wamekuwa wakitumia ardhi ya NAFCO, na kudai kurejeshewa ardhi waliyoipoteza kwa machungu makubwa. Serikali, kwa upande wake imelenga katika kubinafsisha NAFCO na ardhi yake kwa wawekezaji.

Hoja ya wananchi kudai kurejeshewa ardhi waliyoipoteza miaka kadhaa iliyopita ilijitokeza katika Warsha iliyofanyika Mjini Katesh kati ya tarehe 27 – 30 Oktoba 2004. Warsha hii iliwashirikisha wananchi toka kata tatu ambako kuna mashamba ya NAFCO na baadhi ya viongozi na madiwani katika Halmashauri ya wilaya hiyo. Wakati warsha hii inafanyika tayari zilikuwepo taarifa kuwa serikali ilikuwa imeamua kurejesha mashamba mawili kati ya saba kwa wananchi, kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Hanang. Mashamba yaliyoahidiwa kurejeshwa kwa wananchi ni Gawal na Waret. Mashamba mengine matano yataendelea kubinafsishwa kwa mujibu wa nia na mipango ya Serikali.

Mjadala katika warsha hii pamoja na kugusia masuala juu ya uhaba wa ardhi na migogoro itokanayo na uhaba huo na njia mbalimbali za kuitatua, ulijikita zaidi kwenye suala la hatma ya mashamba ya NAFCO. Mjadala juu ya mashamba hayo ulijielekeza


Ng'wanza Kamata

katika masuala makuu matatu; nini kifanyike kwa mashamba yale na kwa nini, nani azingatiwe katika kupata ardhi ya mashamba pindi serikali ikiafiki kuyarejesha kwa wananchi, na nani aamue juu ya ugawaji wa mashamba yale pindi yatakapokuwa yamerejeshwa kwa wananchi.

Juu ya nini kifanyike ilikuwa wazi kuwa wananchi wangependa na kutaka kuona mashamba yote saba yakirejeshwa kwao. Kwa mfano moja ya pendekezo kubwa lililotolewa na kukubalika na washiriki wote wa warsha hii ilikuwa ni kuitaka Serikali irejeshe mashamba yote ya iliyokuwa NAFCO mikononi mwa wananchi. Washirki wa warsha walitamka na kupendekeza kuwa "Kwa vile huko nyuma Serikali ilitwaa ardhi iliyo chini ya mashamba ya iliyokuwa NAFCO wilayani HANANG kwa manufaa ya Taifa kitendo ambacho kilipingwa vikali na wananchi, na kwa vile NAFCO sasa imefilisika na haiitumii tena ardhi yenye mashamba, na kwa sababu wananchi wana shida kubwa ya ardhi kwa ajili ya kuendeleza uzalishaji na kukabiliana na umasikini miongoni mwao, SERIKALI HAINA BUDI KUREJESHA MASHAMBA


***Akinamama Wilayani Hanang wakijadili mustakabali wa ardhi ya mashamba ya NAFCO***



YOTE YALIYOKUWA YA NAFCO KWA WANANCHI."

Pendekezo hili lilitokana na hoja mbalimbali zilizotolewa na washiriki wa warsha hii.

Mmoja wa washiriki alisema "kama suala ni kuitoa ardhi ya NAFCO kwa wawekezaji, sisi pia ni wawekezaji, tunawekeza kidogo kidogo kwa kulima na kufuga. Kwani uwekezaji lazima uwe ni shughuli kubwa tu au kutoka nje? Serikali lazima itutambue sisi pia kama wawekezaji hasa kwenye ardhi." Hoja hii ilifuatiwa na hoja zingine ambazo zilitambua tatizo la uhaba wa ardhi katika maeneo yaliko mashamba ya NAFCO na kutazama urejeshwaji wa mashamba yale kwa wananchi kama suluhu ya tatizo la upungufu wa ardhi. "Ardhi haitoshelezi mahitaji ya watu wa eneo lile, watu wanakuwa squeezed (wanabanwa) na hakuna eneo mbadala" alibainisha mmoja wa Washiriki wa warsha ya madiwani na watendaji wa wilaya. Mshiriki mwingine kwenye warsha hii alisema "Ukisema wilaya ya Hanang hatujaathirika kiasi hicho, husemi kweli/ wafugaji wameondoka kwa sababu ardhi haitoshi." Hoja zote hizi zilitolewa ili kubainisha hoja zilizokuwa zimetokana na taarifa ya utafiti iliyofanywa na HAKIARDHI iliyoonesha kuwa wananchi wengi katika eneo la kata za Basutu, Gehandu na Laghanga walitaja tatizo la uhaba wa ardhi kuwepo na kuwa ardhi kubwa iliyokuwa haitumiki, hususan ile ya mashamba ya NAFCO ingerejeshwa kwa wananchi ingetatua au kupunguza tatizo hilo kwa kiasi kikubwa.

Washiriki wengine, walionyesha hofu juu ya mwekezaji atakayekuja na kama atakuwa na manufaa yoyote kwao. Mshiriki wa warsha iliyowashirikisha wakazi wa kata na vijiji jirani na mashamba ya NAFCO alisema, "huyu mwekezaji atalima kitakachotusaidia?" Suala hili liliibuliwa kutokana na mafunzo na uzoefu walioupata wananchi pale NAFCO ilipokuwa ikilima mashamba ya ngano. Ngano yote iliyozalishwa pale haikukusudiwa kutumika hata kwa kiasi kidogo na wananchi wa maeneo jirani hata pale walipokuwa na upungufu mkubwa wa chakula.

Lakini wengine walitilia hofu juu ya kuongezeka kwa migogoro na misuguano miongoni mwa wananchi kutokana na uhaba wa ardhi. Mshiriki mwingine alisisitiza kuwa "mashamba yote yarejeshwe kwa wananchi vinginevyo uhasama na uhaba utaendelea." Kwa hivyo urejeshwaji wa mashamba ya NAFCO kwa wananchi ulionekana pia kama njia ya kupunguza migogoro ya ardhi baina ya wananchi. Wako walioeleza hofu yao ya jinsi mwekezaji atakayepewa mashamba hayo atakavyoweza kuyaendesha bila kujikuta kwenye mgogoro mkubwa na wananchi kwa vile hamu na matakwa yao siku zote yamekuwa ni kuona ardhi waliyoipoteza siku nyingi ikirejea kwao.

Hoja nyingine iliyotawala majadiliano kwa muda mrefu ni *nani arejeshewe ardhi pindi mashamba yatakapokuwa yamerejeshwa.* Hoja hii ilizua mjadala mkali huku baadhi ya washiriki wakipendekeza ardhi irejeshwe kwa waliokuwa wamepokonywa ardhi ile wakati wa operesheni ya kuwahamisha. Mshirki mmoja mwanamke wa umri wa kati alionelea ni vyema mashamba yakarejeshwa kwa wale waliopokonywa vinginevyo hakuna "kitakachoeleweka". Mshiriki mwingine, mama wa makamo, alionelea ni vyema mashamba yale yakarejeshwa kwa walio karibu na mashamba yale. Hii, kwa mujibu wa mama huyo itawasaidia wale waliopo "kupumua."

Hata hivyo pamoja na tofauti hizi washiriki wa warsha hii hawakupendelea kabisa hoja ya Halmashauri ya wilaya kukabidhiwa mashamba na kwamba yenyewe ndiyo yenye dhamana ya kuamua namna ya kuyagawa. Mshiriki mmoja alipendekeza kuwa "ardhi ile warejeshewe wenyewe walionyang'anywa na wala si Halmashauri." Kimsingi wananchi


ARDHI NI UHAI
ISSN NO. 0856-9495 TOLEO LA 1 Juni 2004
YALIYOMO
Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Ardhi ya 2004
NJAMA ZA KIKABAILA DHIDI YA WANYONGE?
NUKUU YA LEO
"Wakati watu wengi watakapokubali njia ambayo itawawezesha wachache kumiliki kitu ambacho kwa kweli ni zawadi ya mungu kwa watu wote, watakuwa wakiukubali utumwa kwa hiari yao wenyewe."
J.K. Nyerere

walionyesha kutoamini kama watatendewa haki ikiwa Halmashauri ya Wilaya itaachiwa suala zima la kuamua mustakabali wa mashamba yale.

Wananchi walipendekeza kuwa mustakabali na maamuzi juu ya mashamba yale waachiwe wao wenyewe. Pendekezo linalohusiana na jambo hili lilitamka bayana kuwa:

*"Katika kufikiria na kuamua mustakabali wa mashamba ya NAFCO Serikali haina budi kuzingatia kuwa ugawaji wa ardhi/mashamba pindi yatakaporejeshwa kwa wananchi uachwe mikononi mwa wananchi wenyewe kwa kutumia vyombo vyao vyenye uwakilishi mpana kama vile Mkutano Mkuu wa Kijiji ili kutoa haki kwa kila mtu kwa kuzingatia*

**ARDHI NI UHAI! Jarida maridhawa hutolewa mara tatu kwa mwaka.**

**USIKOSE TOLEO LIJALO**

*mahitaji halisi ya wananchi."*

Aidha washiriki walipendekeza kuwa "Ili kuepusha manung'uniko, migogoro na misuguano baina ya wananchi na serikali juu ya ardhi iliyo chini ya mashamba ya NAFCO hatua zozote za kuamua mustakabali wa ardhi iliyo kwenye mashamba hayo hauna budi kuwashirikisha wananchi hususan waishio katika maeneo yaliyo katika mashamba hayo."

Hoja hizi za kutaka ushiriki kamilifu wa wananchi zilitokana pia na "hisia" za Halmashauri kutaka kuamua juu ya hatima ya mashamba ya Gawal na Waret bila hata kuwashirikisha wale waliopokonywa ardhi huko nyuma. Akihoji kujiingiza kwa Halmashauri katika suala hili mshiriki mwingine alisema: "Halmashauri inataka kupata maoni gani ya wadau, ile siyo ardhi iliyoshuka toka mbinguni ina wenyewe, sasa warejeshewe wananchi, ni haki ya watu walioporwa ardhi hiyo hivyo wananchi wenyewe wafanye uamuzi juu ya mashamba yale."

Kwa jinsi yoyote itakavyokuwa ni wazi kuwa suala la upatikanaji na urejeshwaji wa mashamba ya iliyokuwa NAFCO wilayani Hanang litabakia kuwa dai la wananchi kwa muda mrefu ujao. Ni wazi pia, kwa vile sasa ardhi ni rasilimali inayoingizwa kwenye mfumo wa soko na lipo kundi katika jamii linalotaka kujijenga kama tabaka la makabaila, maslahi ya wananchi katika madai ya ardhi ya NAFCO – Hanang yatakuwa katika wakati na mazingira magumu kupatikana. Ni kwa sababu hii 'wakubwa' na wenye nguvu za kisiasa watajijengea na kujiwekea mazingira ambayo yatatoa fursa kubwa kwao kuamua mustakabali wa rasilimali hii kwa maslahi yao kwanza na kwa maslahi ya wananchi kama inalazimu au inabidi, au ni mtaji wa kisiasa kwa wakati uliopo.


*Mmojawapo wa washiriki wa warsha ya masuala ya ardhi wilayani Hanang akijadili mada.*







# MAREKEBISHO YA 14 YA KATIBA NA HAKI YA KUMILIKI MALI

Wataalamu wengi hupenda kuielezea Katiba ya nchi kama mhimili mkuu wa sheria au Sheria mama hasa kwa vile Sheria nyingine yeyote katika nchi husika inapaswa kuzingatia misingi ya ki-Katiba vinginevyo haitakuwa halali. Lakini zaidi ya kuwa Sheria mama Katiba ni chombo muhimu katika nchi ambacho hutoa mwongozo wa kitaifa kuhusu masuala mbalimbali kama vile mifumo ya kisiasa, uchumi na utamaduni, na kuelekeza namna ambavyo rasilimali za taifa na mgawanyo wa Madaraka na Mamlaka vinapaswa kuwa. Hata pale yanapofanyika marekebisho mbalimbali ya Katiba, misingi hiyo muhimu haipaswi kutikiswa ili kulinda ile dhana ya Katiba kuwa mhimili mkuu na mwongozo wa Sheria zote. Lakini pamoja na msisitizo huo, ieleweke kuwa dhana hii ya uhimili wa katiba haiondoi umuhimu wa kuwepo kwa sheria nyingine zinazolinda maslahi muhimu ya wananchi hasa katika kutumia haki yao ya milki juu ya rasilimali na maliasili za taifa lao pale inapobidi kufanya hivyo.

Hivi karibuni serikali imetoa muswada wa mapendekezo ya mabadiliko ya 14 katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977. Madhumuni na sababu za mabadiliko yanayopendekezwa vinaelezwa kuwa ni pamoja na kuondoa dhana ya kuwajibisha Katiba katika Sheria za nchi kwa kuondoa maneno "bila kuathiri masharti ya Sheria nyingine" ili kuimarisha wigo wa demokrasia na kuwezesha utekelezaji wa haki za binadamu. Sababu hizo ni za msingi kwa vile licha ya kupanua wigo wa demokrasia hasa katika mfumo wa utekelezaji na utoaji haki, mabadiliko yanayopendekezwa yanaipa Katiba hadhi yake inayostahili, maana hakuna tena Sheria inayoweza kutungwa ikaleta mashaka ya kuzuia upatikanaji haki iliyotolewa ki-Katiba hususan baada ya kuondolewa maneno hayo.

Hata hivyo, sababu na madhumuni hayo havitakuwa na maana endapo mabadiliko yanayokusudiwa kufanyika yatapora au kuhatarisha upatikanaji wa haki muhimu hasa kwa wananchi wa kawaida kama inavyoashiria katika mapendekezo haya. Upo uwezekano mkubwa wa kuwepo mgongano wa maslahi katika kutekeleza haki za kikatiba na haki ya kumiliki mali kama ardhi kwa mujibu wa sheria za ardhi. Kwa mfano, inapendekelezwa kuwa ibara ndogo ya kwanza katika ibara ya 24 ya katiba ifutwe na kuandikwa upya ili isomeke "kila mtu anayo haki ya kumiliki mali na haki ya hifadhi ya mali yake" na kuondoa maneno bila ya kuathiri masharti ya Sheria za nchi zinazohusika kama ilivyokuwa awali. Kuondolewa kwa maneno hayo kunayafanya masharti yaliyowekwa katika Sheria za ardhi kuhusiana na stahili ya kumiliki rasilimali hiyo muhimu yasiwe na maana tena.

Kwa mujibu wa Sheria ya ardhi Na. 4 ya 1999 kifungu cha 19 (2a-c) na Sheria ya Uwekezaji ya 1997, mtu ambaye si raia wa Tanzania haruhusiwi kumiliki ardhi isipokuwa kwa shughuli za uwekezaji na kwa taratibu zilizowekwa na Kituo cha Uwekezaji (TIC). Haki hiyo ni hafifu na hutambuliwa kitaalamu kama "derivative right" ili kuitofautisha na haki aliyo nayo raia kwenye ardhi ambapo ana haki ya kumiliki ardhi kimila au kwa hati. Hata katika mabadiliko yaliyofanywa katika Sheria ya ardhi mwaka 2004 kifungu cha 3, umewekwa msisitizo kuwa mtu asiye raia ataruhusiwa tu kumiliki ardhi kwa shughuli za uwekezaji na kwa kuingia ubia na raia kwa lengo la kukuza mtaji na kwa taratibu zilizowekwa na kituo cha uwekezaji nchini.

Hivyo mabadiliko ya Katiba yanapotoa idhini ya jumla kuwa kila mtu ana haki ya kumiliki mali na kupata hifadhi ya mali yake na kuondoa sharti la 'kwa mujibu wa Sheria husika', yanaondoa kabisa maana ya masharti yaliyowekwa na Sheria za ardhi kuhusu hakimiliki ya mali hii muhimu ili kutofautisha haki aliyo nayo raia dhidi ya asiye raia.

Ikumbukwe kwamba watu wote waishio katika nchi wakiwemo wasio raia wana haki ya kumiliki mali na hata kupata hifadhi ya mali hiyo. Lakini umiliki wa mali kama gari kwa mfano, ni tofauti na ardhi kwa namna nyingi na wala hauwezi kuwekewa masharti makubwa ya kisheria kama ilivyo kwa ardhi. Kwa vile ardhi imetambuliwa rasmi kisera na kisheria kuwa ni mali yenye thamani, itakuwa vigumu kutekeleza sharti la kisheria kuhusu umiliki wake kwa wasio raia, wakati tayari Katiba ambayo ni Sheria mama inatoa haki hiyo kwa kila mtu. Hofu yangu ni kwamba Katiba ikiliondoa sharti hilo muhimu, uhakika wa hakimiliki (Security of Tenure) juu ya ardhi ya Tanzania kwa wananchi wa kawaida utazidi kutoweka. Hii inatokana na ukweli kwamba, baada ya Sheria za ardhi kurekebishwa na hatimaye kuruhusu uuzaji wa ardhi tupu, (isiyo na maendelezo) milango imefunguliwa kwa wenye vipato vikubwa kununua ardhi kadri wawezavyo kutoka kwa wenye vipato duni. Na kwa vile sasa Katiba inarekebishwa ili kuondoa sharti lililokuwa likizuia wasio raia kumiliki ardhi moja kwa moja, basi uwezekano mkubwa ni kwamba wimbi la walanguzi, waporaji na wanunuzi 'halali' wa ardhi (wageni kwa raia) litazidi kuongezeka na kuimarika na hatimaye kufunika kabisa matumaini ya raia kuishi kwa kutegemea mali na zawadi hii nyeti kutoka kwa Mwenyezi Mungu iitwayo ardhi. Ningependa kutoa rai kwa watunga Sheria wetu kwamba wawe makini kutambua athari za muda mrefu za mabadiliko haya ya 14 ya Katiba hasa kuhusiana na haki ya kumiliki mali. Wakishalitambua hilo wapiganie kurejesha sharti la kwa mujibu wa Sheria husika katika ibara ya 24 ya Katiba ili kuipa Sheria ya ardhi uhai na hadhi inayostahili na kulinda haki na maslahi ya raia wa Tanzania kwenye ardhi yao.



Yefred Myenzi

# BUYUNI WAKATAA KUBURUZWA

*Inatoka uk. 4*

Pamoja na kukubali kusamehe makosa yaliyofanywa na Serikali wanakijiji walitaka zoezi lisimame na wavamizi waondoke mara moja jambo ambalo halikukubaliwa na Mkuu wa Wilaya. Makelele ya HATUTAKI! HATUTAKI! Kupinga Msimamo wa Mkuu wa Wilaya yalilipuka katika hadhara hii na Mkutano ukavunjika.

Pamoja na kuvunjika kwa Mkutano ule ambao haukufikia makubaliano yoyote,

Serikali wilayani ilichukulia Mkutano ule kama tukio la kuhalalisha makusudio ya tangu awali ya kupima viwanja katika eneo la kijiji cha Buyuni II. Harakati za wa wananchi ziliendelea na mbinu mpya za kudhoofisha nguvu yao ya utetezi zilianza. Mathalani, mbali na kutumia vitisho kama vile kuwaita baadhi ya watu kwenye ofisi za wilaya, ulianza mchakato wa kuwabandika majina wale walioonekana kuwa ndio viongozi wa harakati hizo za utetezi. Baadhi ya majina waliyobandikwa ni pamoja na wapinzani, wapinga maendeleo n.k. Nia ilikuwa ni kuwatia hofu na kuwavunja moyo ili wachelee kuendelea na utafutaji wa haki za wanakijiji.Kwa mfano tarehe 8/7/2003 baadhi ya viongozi wa kundi lililokuwa likiendesha harakati za kupinga uvamizi waliitwa Wilayani na kukutanishwa na ujumbe toka Manispaa, Serikali ya Kijiji, na baadhi ya maafisa wa wilaya. Jambo mojawapo lililojadiliwa ni taarifa ya gazeti la Sunday News la tarehe 6/7/2003 lililokuwa na taarifa ya Bunge iliyosema kuwa viwanja vya watu watakaohamishwa kutoka Kipawa vimetengwa Pugu Kajiungeni (viwanja 1700) na Pugu Mwakanga (viwanja 1800). Katika orodha hii Buyuni II haikuwemo. Taarifa hii ya gazeti ilipondwa na hoja nyingine 'mpya' ya kuwa upimaji wa viwanja Buyuni II ilikuwa ni hatua ya kuwapelekea maendeleo watu wa Buyuni II ilitamkwa. Kimsingi Manispaa ilitetea uvamizi wake kwa hoja nyingine na siyo ile ya awali ya kutaka kuwahamishia wananchi wa Kipawa.

> ***Kwa muda sasa kumekuwa na matukio mbalimbali ya uvamizi na majaribio ya kupora ardhi ya wanakijiji wa Buyuni II hatua ambazo zimepingwa vikali na wananchi.***

Hii ilijidhihirisha wazi baadaye pale Manispaa ilipoanza zoezi jingine la kupima viwanja vyake kwa ajili ya maeneo ya kuzikia na Makazi au Ofisi za Manispaa. Wakati hili linaendela Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi nayo ikatumbukiza mradi wa Viwanja 20,000 mkoani DSM - Buyuni II ikipangiwa kutoa viwanja 5,000. Mradi huu nao ulipingwa vikali na wanakijiji wa Buyuni II.

Ufanisi wa uvamizi au majaribio ya kutwaa ardhi ya Buyuni yamesaidiwa sana na mambo mengi yakiwemo haya yafuatayo:- Kwanza, kuonekana kwa mkuu wa Wilaya na vyombo vya dola katika kijiji. Hali hii ilijenga woga miongoni mwa wananchi na kuwavunja nguvu ya kuendelea kudai haki yao. Pili, matamshi ya vitisho toka kwa viongozi, mathalani matamshi kuwa: ardhi yenu itachukuliwa bure mkipinga zoezi hili au serikali imeshika mpini mwanakijiji kashika makali." Tatu, ni vyombo vya habari na propaganda dhidi ya wananchi.

Lakini kwa nini pamoja na Serikali kutumia nguvu na mbinu nyingi kuwadhoofisha wananchi bado upinzani uliendelea? Ziko sababu nyingi ambazo ni pamoja na: Kwanza, taarifa walizokuwa nazo wananchi kuwa eneo la Kijiji cha Buyuni II halihusiki na mradi wa upimaji viwanja kwa ajili ya wakazi wa Kipawa. Wakazi wa kijiji walipata Ramani ya upimaji ambayo ilitamka bayana kuwa eneo lililohusika ni Pugu Mwakanga. Hii iliwapa imani na nguvu ya kuendelea kupinga ukiukwaji wa taratibu na ari ya baadhi ya watendaji na viongozi wa Serikali kufanya mambo kwa msukumo wa maslahi binafsi. Pili, ni kufahamu kwao baadhi ya vipengele vya Sheria ya Ardhi ya Vijiji nambari 5 ya 1999, hususan suala la ushirikishwaji wa wananchi na ufikiaji wa muafaka kwa kufuata ngazi za maamuzi hasa maamuzi katika Mkutano Mkuu wa Kijiji. Ndiyo maana nyakati zote wanakijiji walidai kuitishwa kwa Mkutano Mkuu wa Kijiji jambo ambalo viongozi wa serikali ya kijiji walilikwepa kila mara.

*Inatoka Uk.3*

*uwezekano wa wananchi wa kawaida watumiao ardhi kupokonywa si tu ardhi yao lakini pia uwezo wao wa kuhimili maisha.* Kinyume na matarajio ya kupambana na umasikini mfumo mpya wa ardhi unarahisisha kuenea kwa umasikini hususan pale wanyonge watakaposhindwa kulipa madeni yao na hivyo kumudu mahitaji yao ya msingi.

### Nani Analindwa na Nani Anafaidika?

Dr. R. Mekacha anabaini makundi matatu yanayoathiriwa na mabadiliko ya mfumo wa ardhi. Awali ni wananchi wanaotaka uhakika wa milki za ardhi ili waweze kujikimu; Pili ni makabaila wanaotafuta faida kutokana na kuhodhi au kuiuza ardhi; na mwisho ni wageni wanaotaka kuwekeza na kupata faida. Uhakika wa hati miliki wa wananchi walio wengi umeshindikana na maelefu ya ekari za ardhi zimeporwa kutoka kwa wanavijiji na kukabidhiwa kwa wamiliki wakubwa wengi wakiwa wawekezaji kutoka nje hali ambayo imeleta taathira mbaya kwa jamii husika.

Kwa upande wake Prof.. Koda anaona mabadiliko makubwa kuhusiana na upatikanaji ardhi, uhamishaji ardhi, umiliki ardhi na udhibiti ardhi katika miongo ya karibuni. Mabadiliko haya yameleta taathira kwa mahusiano ya kinyumba na kijamii. Prof. Koda anaamini kwamba haki za wanawake kumiliki ardhi na mafao yao zimepotea wakati wa ukoloni na baada ya uhuru. Anasema, "utaratibu wa kuibinafsisha ardhi na kuifanya kuwa bidhaa ili kukidhi haja za mabadiliko ya kiuchimu duniani imefanya kuwepo kwa changamoto za kipekee kijinsia na kitabaka".

Katika ubinafsishaji huu wa ardhi nani analindwa? Prof. Chachage anahusisha kuja kwa wawekezaji katika miaka ya themanini na suala zima la mabadiliko katika mfumo wa umiliki wa ardhi nchini, jambo ambalo limechangia sana katika kuleta migogoro ya ardhi na mali asili. Katika kipindi hiki ardhi imekuwa ikihamishwa toka kwa wananchi kwenda kwa watu binafsi, ukiachilia mbali uhamishaji mkubwa wa ardhi uliofanyika wakati wa operesheni Vijiji mwanzoni mwa miaka ya sabini. Kwa kiasi kikubwa mfumo wa uchumi huria umesababisha kuwepo kwa matabaka na mivutano kijamii.

> ***mfumo wa umilikaji ardhi wa sasa una kinzana katika mtizamo wake wa maendeleo na suala zima la demokrasia.***

Jamii ya Kimasai na jamii nyingine za wafugaji na wawindaji, kwa mujibu wa Prof. Chachage na wakereketwa wa masuala ya ardhi, ndizo zilizoathirika zaidi na uporaji ardhi.

Wengi wamehamishwa kutoka maeneo yao ya jadi yenye malisho mazuri na kuhamishiwa kwenye maeneo kame na yasiyo na malisho. Matokeo yake ni kuwaweka katika wakati mgumu wafugaji na hivyo kuwawia vigumu kumudu maisha yao kwa kutegemea mifugo peke yake katika mazingira mapya.

### Ardhi na Maendeleo

Kuna mgawanyiko wa kifikra kati ya dira ya maendeleo na sababu za kubadilisha sera ya ardhi. Sasa madhumuni ya ardhi si tu kwa ajili ya kuhakikisha upatakanaji wa chakula au uhakika wa miliki ila ni kwa madhumuni ya kuwezesha uwekezaji. Wakati umuhimu wa uhakika wa chakula unatambulika kitaifa inashangaza kwamba suala hili halihusishwi na uwezo wa wanawake kumiliki ardhi kwani wanawake ndio wakulima wakuu. Vilevile suala la ufugaji ingawa ni sekta ya kiuchumu bado halipewi uzito unaostahili.


Kwa mujibu wa Mwanasheria Bi. Ndonde mfumo wa umilikaji ardhi wa sasa unakinzana katika mtizamo wake wa maendeleo na suala zima la demokrasia. Kwa upande mmoja unaona maendeleo kama ni mahusiano ya kiuchumi yanayowezeshwa na soko huria na vitega uchumi kutoka nje, na kwa upande mwingine ni mfano wa demokrasia kati ya wananchi na dola. Kiini cha fukuto la migogoro ya ardhi hakihusiani tu na suala la wananchi kujikimu lakini suala zima la mustakabali wao. Iwapo mahitaji ya wananchi ya sasa na ya baadaye hayatazingatiwa katika mipango ya maendeleo kutaendelea kuwepo kwa migogoro ya ardhi na rasilimali zake kati ya makundi mbalimbali kila mmoja akidai haki yake ya ardhi na mafao yake.

# MACHAPISHO

| Na. | Jina la Kitabu | Mwandishi |
|---|---|---|
| 1. | Not Yet Democracy: *Reform land tenure in Tanzania - 1998* | Issa G. Shivji |
| 2. | Ardhi ni Uhai - *1995* | Georgios Hadjivayanis |
| 3. | Mwongozo wa Haki za Ardhi kwa Wananchi wa Tanzania - *2002* | Issa G. Shivji/ Deus Kibamba |
| 4. | Fukuto la Migogoro ya Maeneo na Hatma ya Wazalishaji Wadogo Wadogo Tanzania - *2002* | Aida Isinika (Mhariri) |
| 5. | Msukumo na Harakati za Kubadili Mfumo wa Umilikaji Ardhi Tanzania - *2000* | Ng'wanza Kamata (Mhariri) |
| 6. | Maasai Rights in Ngorongoro, Tanzania - *1998* | Issa G. Shivji & Wilbert Kapinga |
| 7. | Haki za Wamaasai waishio hifadhi ya Ngorongoro *1999* | Issa G. Shivji, Wilbert Kapinga, |
| 8. | Mfumo wa Umilikaji Ardhi Tanzania, *1997* | Issa G. Shivji and Wilbert Kapinga (Wahariri) |



***Machapisho ni nyenzo muhimu katika kutoa mafunzo kuhusu haki za ardhi kwa wananchi hususan waishio vijijini. Pichani watoto Bhoke R. Mekacha na Timothy B Kaare wakizindua Mwongozo wa mafunzo ya Haki za Ardhi kwa wananchi na kitabu kuhusu Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi vilivyochapishwa na HAKIARDHI.***




**Karibuni kwenye semina zetu za kila mwezi jengo la umoja wa vijana barabara ya Morogoro. Wasiliana nasi (hasa kwa barua pepe au simu) ili tukujulishe tarehe za semina.**

H A K I A R D H I

A R D H I N I U H A I

HAKIARDHI



*"Tukiruhusu ardhi iuzwe kama kanzu, katika muda mchache kutakuwa na kundi dogo la watu wenye ardhi na walio wengi watakuwa watwana... wahenga waliepuka hatari hii kwa kukataa kugawa ardhi kwa msingi wa mali binafsi"*

*Mwl. J. K. Nyerere, 1958*

**Anuani/Ofisi**

Taasisi ya Utafiti na Utetezi wa Haki za Ardhi **(HAKIARDHI)**,
Br. Morogoro , Jengo la Vijana , Chumba na. 4,
Ghorofa ya mwisho.

S.L.P. 75885,
Dar es Salaam, Tanzania.
Simu/Faxi +255 22 2152448, +255 748 646 752.
E-mail: hakiardhi@raha.com/info@hakiardhi.org
Tovuti:www.hakiardhi.org

Chapa na **Ecoprint Ltd**, Barua pepe: ecoprint@raha.com